



**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**



**TANGAZO LA FURSA ZA MAFUNZO YA UKUZAJI UJUZI KATIKA FANI ZA  
UMEME VIWANDANI, UFUNDI VIPURI, UFUNDI MAJOKOFU NA  
VIYOYOZI, UTAYARISHAJI VYAKULA NA NISHATI YA JUA**

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) inatangaza nafasi za mafunzo ya ufundi stadi KATIKA FANI ZA UMEME VIWANDANI, UFUNDI VIPURI, UFUNDI MAJOKOFU NA VIYOYOZI, UTAYARISHAJI VYAKULA NA NISHATI YA JUA (SOLAR) kwa vijana wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35.

Mafunzo hayo yanatolewa kupitia Mradi wa Kukuza Ujuzi, Majadiliano ya Kijamii na Ajira zenye staha kwa Vijana wa Kitanzania, unaofadhiliwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Denmark (DTDA) kwa kushirikiana na Shirikisho la Viwanda Denmark (DI), DFPA na kuratibiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Chama Cha Waajiri Tanzania (ATE).

**UGHARAMIAJI MAFUNZO**

Mafunzo kwa vijana wataochaguliwa yatagharamiwa na mradi.



**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

**VETA MAKAO MAKUU**

Kiwanja Na. 18, Central business Park (CBP)  
S. L. P. 802,  
DODOMA.

+255 755 267 489



## VYUO VITAKAVYOTOA MAFUNZO

Mafunzo hayo yatatolewa katika vyuo vya VETA na Don Bosco kama ifuatavyo:

1. Chuo cha VETA Dar es salaam

S.L.P. 40274, Dar es Salaam.

Eneo kilipo: Barabara ya Chang'ombe

Simu: 022 2862562 au 0626 791 685 - Mratibu wa Kozi Fupi

Barua pepe: [dsmrvtsc@veta.go.tz](mailto:dsmrvtsc@veta.go.tz).

2. Chuo cha VETA Mikumi

S.L.P 110, Mikumi.

Eneo kilipo: Mikumi mjini, mkoa wa Morogoro.

Simu: 023 2620458.

Barua pepe: [mikumivtc@veta.go.tz](mailto:mikumivtc@veta.go.tz).

3. Chuo cha VETA Kihonda

S.L.P. 2208, Morogoro.

Simu : 023 2603734.

4. Don Bosco Oysterbay VTC,

2165 Mbuyuni Oysterbay, Barabara ya Ali Hassani Mwinyi

Simu: 0699 116 395

Barua pepe: [info@donboscoyesterbay.co.tz](mailto:info@donboscoyesterbay.co.tz)

## **MUDA WA MAFUNZO**

Mafunzo yatafanyika kwa kipindi cha miezi minane (8) ikiwa imegawanywa katika maeneo mawili: Mafunzo chuoni, miezi sita (6) na Mafunzo ya vitendo sehemu ya kazi, miezi miwili (2).

Maombi ya kujiunga na Mafunzo yapelekwe kwenye vyuo kwa kujaza Fomu ya Maombi. Fomu za Maombi zinapatikana kwenye vyuo husika.

## **VIGEZO VYA KUJIUNGA NA MAFUNZO.**

Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:

- I. Awe raia wa Tanzania
- II. Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 35
- III. Aweze tayari kuhudhuria mafunzo katika vyuo husika
- IV. Awe na elimu ya kidato cha Nne au umeajiriwa katika fani husika

## **JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Maombi yatumwe kwenye vyuo husika (kama vilivyoorodheshwa). Muombaji anatakiwa atume barua ya maombi ikitaja fani anayoomba. Barua ya maombi iambatishwe na nakala za nyaraka zifuatazo:

- I. Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Taifa au leseni ya udereva au kitambulisho cha kura
- II. Barua ya utambulisho kutoka Serikali za Mtaa na
- III. Cheti cha kidato cha Nne au barua ya muajiri.

## **MUDA WA MAOMBI NA USAILI WA WAOMBAJI**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 16 Desemba 2022. Usaili wa Waombaji utafanyika kati ya tarehe 19 Desemba mpaka 13 Januari 2023.

## **KUANZA KWA MAFUNZO**

Mafunzo yanatarajiwa kuanza 16 Januari 2023.

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na Vyuo husika.**